Elimu bora au bora elimu?

Elimu waitakayo watanzania.

1. Utangulizi

Elimu bora ina faida kubwa kwa maisha ya kila siku ya wananchi na pia huchangia ukuaji wa uchumi[1]. Kwa kutambua hilo, serikali nyingi katika nchi zinazoendelea na zile zenye uchumi wa kati zimeweka Elimu kuwa kipaumbele katika mipango ya maendeleo. Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo, na serikali ya awamu ya tano imeipa kipaumbele Sekta ya elimu. Kwa mfano, Serikali ilitenga shilingi za kitanzania trilioni 2.1 kwa sekta ya elimu katika mwaka wa fedha 2017/18 ukilinganisha na shilingi za kitanzania trilioni 1.7 zilizotengwa mwaka 2015/2016[2].

Juhudi kubwa za serikali zimekusudia kupanua wigo wa upatikanaji wa elimu ya msingi kwa kuondoa vikwazo kama vile ada na michango ya wazazi kwenye elimu ya awali, shule za msingi mpaka kidato cha nne. Hivi karibuni, Rais John Pombe Magufuli amerudia kuelezea msimamo wa serikali wa kutoa elimu bure, na kutoa onyo kwa maafisa elimu ambao watashindwa kutekeleza sera hiyo[3].

Serikali pia imetambua umuhimu wa kuboresha viwango vya elimu ili kuendana na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi. Juhudi za hivi karibuni zimekusudia kuboresha stadi za msingi za kuhesabu, kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa darasa la 2, kuboresha mfumo wa kuhakiki ubora wa elimu, kuwezesha wanafunzi kumaliza shule na kuongeza idadi ya wasichana wanaojiunga na elimu ya sekondari.

1 Hanushek, Eric A. and Woessmann, Ludger, The Role of Education Quality for Economic Growth (February 1, 2007). World Bank Policy Research Working Paper No. 4122. Available at SSRN: https://ssrn.com/abstract=960379

2 http://www.mof.go.tz/mofdocs/budget/Citizens%20Budget/CITIZENS%20BUDGET%202017_18%20%20%20%20%20%20(Eng_Final).pdf

3 https://dailynews.co.tz/index.php/home-news/55438-jpm-spits-fire-on-school-charges

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania. +255 22 266 4301 | info@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

Pamoja na malengo mazuri ya sera hii ya elimu bila malipo ya ada iliyoagizwa na waraka wa elimu namba 5 wa mwezi Disemba mwaka 2015, bado kuna changamoto katika upatikanaji na ubora wa elimu nchini Tanzania.

Muhtasari huu unawasilisha maoni ya wananchi kwenye masuala haya na masuala yanayohusiana na sera ya elimu. Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* ambao huratibiwa na taasisi ya Twaweza. Kwenye utafiti huu, maswali kadhaa yaliulizwa ikiwemo: Je, wazazi wangependa kulipa ada iwapo ubora wa elimu utaongezeka? Ni kwa kiasi gani wazazi wanajihusisha na elimu ya watoto wao? Na ni kwa kiasi gani wanafahamu matokeo ya shule zilizoko kwenye maeneo yao?

Sauti za Wananchi ni utafiti unaotumia simu za mikononi na una uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Zanzibar haihusiki kwenye utafiti huu. Taarifa zaidi kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kwenye tovuti ya Twaweza www.twaweza.org/sauti. Takwimu hizi zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,786 katika awamu ya 23 ya kundi la pili la *Sauti za Wananchi*, na zilikusanywa kati ya tarehe 25 Septemba na tarehe 15 Oktoba mwaka 2017.

Awamu hii ya utafiti ilifanyika kwa ushirikiano na Utafiti wa Kuboresha Mifumo ya Elimu (RISE) nchini Tanzania.[4]

Matokeo muhimu ni:

- Watoto kutoka kaya 9 kati ya 10 nchini Tanzania wanasoma shule za serikali.
- Wazazi 9 kati ya 10 wangependelea kulipa ada ili kupata elimu bora kuliko kutokulipa ada, na kupata elimu isiyo bora.
- Karibu wazazi 9 kati ya 10 wangechagua mpango wa serikali wa kutoa mafunzo na kuwawezesha walimu kuliko mpango wa kugawa bure sare za shule.
- Asilimia 85 ya wazazi walikutana na walimu wa watoto wao angalau mara moja katika mwaka uliopita; kuna ongezeko ukilinganisha na mwaka 2016.
- Wazazi waliowengi (53%) walichangia fedha, vifaa na/au nguvu kazi katika ujenzi wa shule mwaka uliopita.
- Uelewa wa wazazi kuhusu ufaulu wa shule za msingi mara nyingi hutofautiana na uhalisia.
- Zaidi ya nusu ya wazazi wanasema husaidia uongozi wa shule kwa kuwaadhibu watoto wao.
- Mzazi 1 kati ya 20 pekee ndiye huzingatia ada nafuu kama kigezo cha kuchagua shule ya sekondari kwa ajili ya mtoto wake.

4 RISE ni mradi mkubwa wa utafiti wa nchi mbali mbali ambao unatafuta kuelewa jinsi ambavyo mifumo ya shule katika nchi zinazoendelea inaweza kutatua mgogoro wa kujifunza ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora kwa wote. Twaweza ni mshirika wa kitaasisi na mwanachama wa jumuiya za taasisi zinazohusika kwenye mradi wa utafiti wa RISE hapa Tanzania.

2. Mambo nane muhimu kuhusu elimu ya umma nchini Tanzania

Jambo la 1: Watoto wengi nchini Tanzania wanasoma shule za serikali

Elimu nchini Tanzania inatolewa zaidi na sekta ya umma. Kaya tisa kati ya kumi (90%) zimesema kuwa watoto wao wanasoma shule za serikali.

Idadi ya kaya zenye mtoto anayesoma shule binafsi imebaki pale pale (10% tu) kati ya mwezi Agosti mwaka 2016 na Septemba mwaka 2017. Wakati kaya tisa kati ya kumi kwa sasa hazina watoto wanaosoma shule binafsi, zaidi ya nusu (52%) wanasema kuwa wangewapeleka watoto wao kwenye shule binafsi badala ya shule za serikali kama shule zote zingekuwa bure.

Kielelezo cha 1: Watoto wanaosoma shule binafsi na shule za serikali kuanzia shule za awali mpaka kidato cha nne[5]



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 5 (Disemba 2016-Januari 2017; n=1,179), awamu ya 10 (Agosti 2016; n=1,457) na awamu ya 23 (Septemba-Oktoba 2017; n=1,396)

Kielelezo cha 2: Watoto wanaosoma shule binafsi na shule za serikali: kwa kiwango cha elimu



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Septemba-Oktoba 2017); Msingi: kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma kwenye aina hiyo ya shule

Jambo la 2: Wananchi wengi wangependa kulipia ubora

Karibu wananchi tisa kati ya kumi (87%) wanasema wangependa kulipa ada kwa ajili ya kupata elimu bora, kuliko kutokulipa ada na kupata elimu isiyo bora. Ukilinganisha na takwimu kutoka

5 "Binafsi / Zote" inajumuisha kaya zenye mtoto mmoja au zaidi wanaosoma shule binafsi.

tafiti za Afrobarometer[6] mwaka 2001-2005, mitazamo ya wananchi kuhusu ada imebadilika, hapo awali wananchi wengi waliunga mkono upatikanaji wa elimu bure.

Ni muhimu kufahamu kuwa maswali ya tafiti hizi hayaelezi maana ya elimu yenye ubora wa hali ya juu wala hayaelezi ni gharama kiasi gani wananchi watapaswa kulipa. Hata hivyo, matokeo yanaonesha kuwa wananchi wengi wana mashaka na ubora wa elimu inayotolewa hivi sasa na wako tayari kulipa gharama ili kupata matokeo mazuri.

Kielelezo cha 3: Elimu bure isiyo na ubora au elimu ya kulipia yenye ubora



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017; n=1,786) na tafiti za Afrobarometer awamu ya 1 (2001; n=2,198), awamu ya 2 (2003; n=1,223) na awamu ya 3 (2005; n=1,304)

Jambo la 3: Wananchi 9 kati ya 10 wanachagua mafunzo kwa walimu badala ya kupewa sare za shule bure

Walipoulizwa iwapo wangependa mpango wa serikali wa kugawa sare za shule bure kwa watoto wao au mpango wa kutoa mafunzo ya ziada na kuwasaidia walimu, wananchi tisa kati ya kumi (87%) walichagua mpango wa kutoa msaada na mafunzo kwa walimu. Hii inaongeza ushahidi zaidi kwenye wazo kuwa wananchi wanapendelea jitihada ambazo zitaboresha elimu kuliko zile zinazopunguza gharama ya elimu.

Kielelezo cha 4: Je, ungependa mpango wa serikali unaogawa sare za shule bure ili usinunue nguo hizo tena, au mpango wa kutoa mafunzo na msaada kwa walimu ili wafundishe vizuri darasani?



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017; n=1,786)

6 Angalia Afrobarometer.org

Jambo la 4: Nusu ya wazazi walichangia ujenzi wa shule mwaka uliopita

Zaidi ya nusu ya wazazi wenye watoto wanaosoma shule za msingi wanasema walichangia ujenzi wa shule mwaka uliopita. Takribani wazazi wanne kati ya kumi (38%) walichangia fedha, wakati mzazi mmoja kati ya kumi (9%) alichangia vifaa na wazazi wawili kati ya kumi (18%) walichangia nguvu kazi wakati wa ujenzi.

Kielelezo cha 5: Wewe au yeyote kwenye kaya yako alichangia nini katika ujenzi wa shule mwaka huu?
(*jibu zaidi ya moja linaruhusiwa miongoni mwa waliochangia)*



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017); Msingi: kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi (n=1,209)

Wazazi pia walitoa michango mingine ya fedha shuleni. Karibu kaya zote zenye mtoto anayesoma shule ya msingi (99%) zilinunua vifaa kwa ajili ya mtoto/watoto wao mwaka uliopita. Vitu ambavyo wanasema walinunua ni vifaa vya kuandikia (98%), nguo za shule (75%), mabegi ya shule (26%) na vitabu (15%).

Kielelezo cha 6: Ni vifaa gani vya shule wewe au mtu kwenye kaya yako alinunua kwa ajili ya mwanao mwaka huu?



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017; Msingi: kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi (n=1,209)

Jambo la 5: Wazazi 7 kati ya 8 wa wanafunzi wa shule za msingi walikutana mara moja au mbili na walimu mwaka uliopita

Wazazi saba kati ya nane wenye watoto wanaosoma shule za msingi (85%) wanasema walikutana na walimu wa watoto wao angalau mara moja au mbili mwaka uliopita – na karibu idadi sawa (86%) wanasema kuwa walitembelea shule za watoto wao angalau mara moja katika kipindi hicho

hicho (haijaoneshwa kwenye jedwali). Idadi ya kukutana kwa mzazi na mwalimu imeongezeka kutoka mwaka 2016 hadi 2017.

Kielelezo cha 7: Katika mwaka uliopita, mara ngapi umekutana na mwalimu wa mtoto/watoto wako?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi – awamu ya 10 (Agosti 2016; n=1,391) na awamu ya 23 (Septemba-Oktoba 2017; n=1,209)

Jambo la 6: Wazazi wengi hawana uelewa sahihi juu ya ubora wa ufaulu katika shule zilizopo wanapoishi

Wazazi wanaoishi vijijini ambao watoto wao wanasoma shule za msingi hawana uelewa wa kutosha kuhusu matokeo ya shule zilizoko kwenye maeneo yao. Pamoja na jitihada zilizofanywa na serikali hivi karibuni za kusambaza matokeo ya mtihani wa kuhitimu darasa la saba na kidato cha nne, utafiti huu umeonesha bado kuna tatizo katika ufikishaji wa taarifa.

Hususani, upo utofauti mkubwa kati ya mapokeo na tafsiri ya wazazi kuhusu matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba na matokeo halisi[7]: pale ambapo shule yao ya msingi ina matokeo mabaya (chini ya 51% ya ufaulu), wazazi wengi (56%) wanasema matokeo ya shule zao ni *mazuri* au *mazuri sana*. Ni 5% tu ya wazazi hawa waliosema matokeo ya shule zao ni *mabaya* au *mabaya sana*. Vile vile, kwa upande mwingine, pale ambapo shule ya msingi ina kiwango kizuri sana cha ufaulu (juu ya 91%), ni 15% tu ya wazazi waliosema matokeo ya shule "ni mazuri sana," wakati robo yao (26%) wakisema ni ya *wastani* au *mabaya*.

Kielelezo cha 8: Mitazamo ya wazazi kuhusu matokeo ya shule zilizoko kwenye maeneo yao ukilinganisha na matokeo halisi

Kwenye shule ambazo zina matokeo mazuri sana (kiwango cha ufaulu zaidi ya 91%), ni kwa kiasi gani wazazi wanafahamu kuhusu kiwango cha ufaulu wa shule hizo?



7 Kaya ziliulizwa kuhusu viwango vya ufaulu katika shule wanazosoma watoto walio wengi katika kijiji chao

Kwenye shule ambazo zina matokeo mabaya sana (kiwango cha ufaulu chini ya 51%) , ni kwa kiasi gani wazazi wanafahamu kuhusu kiwango cha ufaulu wa shule hizo?



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017; Msingi: kaya za vijijini zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi (n=503)

Jambo la 7: Usimamizi wa nidhamu ndio msaada mkubwa unaotolewa na wazazi kwenye uongozi wa shule

Kaya zenye watoto wanaosoma shule za msingi huwaadhibu watoto wao kama njia mojawapo ya kuusaidia uongozi wa shule (52%). Wazazi pia husaidia katika harambee za kukusanya fedha (22%) au kufuatilia mahudhurio ya walimu (14%). Kaya moja kati ya nne zenye watoto wanaosoma shule za msingi (24%) hawatoi msaada wowote kwa uongozi wa shule.

Kielelezo cha 9: Tafadhali onesha njia zote ambazo wewe au watu wengine kwenye kaya yako walitumia kutoa mchango wao kwa uongozi wa shule



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017; Msingi: kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi (n=1,209)

Pamoja na haya, idadi kubwa ya wazazi (52%) wanaona wana wajibu wa msingi wa kuhakikisha watoto wao wanajifunza wakati 46% ya wazazi wanasema walimu wana wajibu zaidi. Hakuna wazazi waliotaja viongozi wa shule, maafisa waliochaguliwa au maafisa wengine wa serikali wanaohusika na kujifunza kwa watoto (haijaoneshwa kwenye majedwali).

Jambo la 8: Mzazi 1 kati ya 20 pekee ndiye huzingatia ada nafuu kama kigezo cha kuchagua shule ya sekondari kwa ajili ya mtoto wake.

Wazazi wenye watoto wanaosoma shule za msingi huzingatia matokeo mazuri ya mtihani wa kidato cha nne (72%) na walimu wenye ari (72%) kama sifa mbili kuu wanapotafuta shule ya sekondari kwa ajili ya watoto wao. Sifa nyingine muhimu kwa kaya ni miundombinu mizuri (54%) na sifa nzuri ya shule (38%).

Ni mzazi mmoja tu kati ya ishirini (6%) anayetaja ada nafuu kama kigezo cha uchaguzi wa shule na wazazi wanne kati ya ishirini (18%) huzingatia ukaribu wa shule na maeneo wanapoishi. Hii

inaonesha kuwa wazazi huzingatia zaidi ubora wa elimu ya sekondari ambayo mtoto wao anapata kuliko ada au umbali wa shule.

Kielelezo cha 10: Ni sifa gani tatu muhimu zaidi huzingatia wakati wa kuchagua shule ya sekondari?



Chanzo cha takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 23 (Sept-Okt 2017); Msingi: kaya zenye angalau mtoto mmoja anayesoma shule ya msingi (n=1,209)

3. Hitimisho

Wazazi wameongea kwa uwazi; wanajali zaidi ubora wa elimu kuliko gharama za kuipata elimu hiyo. Inawezekana kwamba mtazamo huu unetokana na changamoto za sasa katika sekta ya elimu kufuatia ongezeko la idadi ya watoto shuleni baada ya kufutwa kwa ada. Ni vema viongozi wa ngazi zote wakayazingatia maoni haya ya wananchi wakati wa kuandaa na kutekeleza sera za elimu.

Wazazi wanaendelea kuchangia ujenzi mashuleni; hata hivyo takwimu hizi zilikusanywa kabla ya msisitizo wa hivi karibuni kuwa michango ya hiari inayotolewa na wazazi ipelekwe kwenye mamlaka za wilaya na siyo kwenye shule[8]. Na vile vile kuna ongezeko la idadi ya wananchi wanaosema kuwa walikutana na mwalimu wa mtoto au watoto wao mara moja au mbili mwaka uliopita. Pengine sasa wazazi wanajitahidi kujihusisha na kushirikiana na shule za umma.

Hata hivyo, bado kuna pengo katika upataji wa taarifa. Utafiti wa hivi karibuni wa Twaweza[9] umeonesha kuwa pale ambapo wazazi wanapata taarifa, wanaweza kushiriki ipasavyo kwenye maamuzi na wanapokaribishwa shuleni na kwenye michakato ya shule, hujiona wakihusika zaidi na elimu ya watoto wao, na wanakuwa na utayari zaidi na uwezekano wa kuchukua maamuzi ya kusaidia shule. Na hivi karibuni utafiti wa kimataifa umeonesha kwamba ushiriki wa wazazi kwenye uongozi wa shule ni nguzo muhimu katika kuhakikisha watoto wanajifunza shuleni[10].

Labda kwa kusikiliza sauti za wazazi na kuwawezesha kujihusisha na masuala ya shule, Tanzania inaweza kupiga hatua kubwa katika kuhakikisha watoto wote wanapokea haki yao ya kupata elimu bora.

8 https://www.dailynews.co.tz/index.php/home-news/55438-jpm-spits-fire-on-school-charges
9 Haujachapishwa
10 World Development Report 2018 http://www.worldbank.org/en/publication/wdr2018